**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

**AGENDA ZA MKUTANO WA TATU KIKAO CHA PILI CHA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI), 2022/2023.**

**SIKU YA PILI YA MKUTANO TAREHE: 19/05/2023**

6. Maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Mstahiki Meya na Mkurugenzi.
7. Kupokea taarifa ya Mkurugenzi.
8. Kupokea taarifa toka kwa Mstahiki Meya.
9. Salam kutoka Serikali Kuu.
10. Salam kutoka Chama cha Mapinduzi.
11. Kupokea taarifa za utekelezaji kutoka Kamati za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.
    i. Kamati ya Mipango Miji.
    ii. Kamati ya huduma za Elimu, Uchumi na Afya.
    iii. Kamati ya Ukimwi.
    iv. Kamati ya Fedha na Uongozi.
12. Kupitia utekelezaji wa maagizo ya (CAG) kuhusu hoja za ukaguzi maalumu.
13. Mengineyo.
14. Kufunga Mkutano.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

# MUHTASARI WA MKUTANO WA PILI KIKAO CHA PILI CHA BARAZA LA MADIWANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI (OKTOBA-DISEMBA), 2022/2023 KILICHOFANYIKA TAREHE 01 FEBRUARI, 2023, KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA DDC

## MAHUDHURIO

### a) Wajumbe waliohudhuria

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Mh, Frank Magali | Mstahiki Meya | | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe, Salum Bakari Ng`ondo | Diwani | Nangaru- Naibu Meya | Mjumbe |
| 3. | Mhe, Nyanga M. Nyanga | Diwani | Tandangongoro | Mjumbe |
| 4. | Mhe, Khalfan M. Mandanje | Diwani | Nachingwea | Mjumbe |
| 5. | Mhe, Asina Y. Kawanga | Diwani | Msinjahili | Mjumbe |
| 6. | Mhe, Mwanajuma Amiri | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 7. | Mhe, Lunda J. Lunda | Diwani | Makonde | Mjumbe |
| 8. | Mhe, Jumu A. Ndondi | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 9. | Mhe, Mwanaidi D. Mbungo | Diwani | Ng`apa | Mjumbe |
| 10. | Mhe, Athuman I. Mmaije | Diwani | Rutamba | Mjumbe |
| 11. | Mhe, Yahya O. Mohamed | Diwani | Mvuleni | Mjumbe |
| 12. | Mhe, Zuhura B. Matindila | Diwani | Kitomanga | Mjumbe |
| 13. | Mhe, Kasim A. Namwete | Diwani | Kilangala | Mjumbe |
| 14. | Mhe, Hussein S. Kimbyoko | Diwani | Milola | Mjumbe |
| 15. | Mhe, Meja K. Seleman | Diwani | Kilolambwani | Mjumbe |
| 16. | Mhe, Abdallah O. Mtambule | Diwani | Kiwawa | Mjumbe |
| 17. | Mhe, Asha Y. Mkukulu | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 18. | Mhe, Sharifa S. Kambanga | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 19. | Mhe, Esha S. Mpwaga | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 20. | Mhe, Niger C. Mpetula | Diwani | Mingoyo | Mjumbe |
| 21. | Mhe, Said M. Mchinjita | Diwani | Mnazimmoja | Mjumbe |
| 22. | Mhe, Abeid B. Abeid | Diwani | Mtanda | Mjumbe |
| 23. | Mhe, Kitutuma A. Abdurahman | Diwani | Rahaleo | Mjumne |
| 24. | Mhe, Mariam S. Chande | Diwani | Wailes | Mjumbe |
| 25. | Mhe, Idd Ngunde | Diwani | Matopeni | Mjumbe |
| 26. | Mhe, Paul L. Mapunda | Diwani | Mwenge | Mjumbe |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27. Mhe, Abdallah N. Thabit | Diwani | Mbanja | Mjumbe |
| 28. Mhe, Rashid S.Rashid | Diwani | Jamhuri | Mjumbe |
| 29. Mhe, Seleman T Laus | Diwani | Mitandi | Mjumbe |
| 30. Mhe, Fatuma A. Said | Diwani | Chikonji | Mjumbe |
| 31. Mhe, Abdallah Kikwei | Diwani | Rasbura | Mjumbe |
| 32. Mhe, Juma S. Mpendakulya | Diwani | Ndoro | Mjumbe |
| 33. Mhe, Seif Said Njenga | Diwani | Mipingo | Mjumbe |
| 34. Mhe, Mswalile I. Ally | Diwani | Mchinga | Mjumbe |
| 35. Mhe, Twahil A. Mpuluji | Diwani | Matimba | Mjumbe |
| 36. Mhe, Zainabu Fundi | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 37. Mhe, Hamida I. Mnunguye | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 38. Mhe, Fatuma Seleman Ussy | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 39. Mhe, Ashiza Abdallah | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |
| 40. Mhe, Zahara Hassan | Diwani | Mikumbi | Mjumbe |
| 41. Mhe, Semeni J. Ally | Diwani | Viti Maalum | Mjumbe |

**b). Wajumbe wasiohudhuria**

1. Mhe, Salma Rashid Kikwete — Mbunge Jimbo la Mchinga – kwa taarifa
2. Mhe, Hamida Abdallah — Mbunge Jimbo la Lindi Mjini – Kwa taarifa

**c). Wataalam waliohudhuria**

1. Ndg. Stanford Mwakatage — Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa - Katibu
2. Emmanuel Lweyo — Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi Rasilimali watu.
3. Carlos Kanyopa — Afisa Utumishi.
4. Jamali Lisuma — Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Michezo, Utamaduni na Sanaa.
5. Eng. Nestor Chialo — Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundo Mbinu Vijijini na Mjini.
6. Ezekiel M.Sumbuka — Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira.
7. Salehe Mohamedi — Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma ya Sheria.
8. Dkt Ninzar Idd — Mkuu wa Idara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.
9. Seif A seif — Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Taka na Usafi wa Mazingira.
10. Dativa A Kyssima — Mratibu wa TASAF.
11. Bakari A Abdallah — Afisa Lishe

12. Imani Komba - Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii.
13. Alex A Mkwango - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Awali na Msingi
14. Osward R Winston - Afisa Ardhi
15. Florence Kalimwa - Kaimu Mkuu wa Idara ya Usimamizi wa Manunuzi
16. Tatu Omari Seif - Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
17. Mwandishi Nchimbi - Mkuu wa Idara ya Mipango,Uratibu na Takwimu
18. Nasri Mchekenje - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Serikalini.
19. Faidha S Kassim - Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
20. Rehema Nahale - Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari.
21. Omari Furaha - Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo,Mifugo na Uvuvi.
22. Abilah Mbingu - Kaimu Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma ya Lishe.
23. Neema Sabuni - Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Fedha na Uhasibu.
24. Abdallah Chiako - Afisa Tarafa Nangaru
25. Sharifa Mkwango - Afisa tarafa Lindi Mjini
26. Christina Chiwanga - Kaimu Afisa tarafa Mingoyo
27. Maimuna Kawimba - Kaimu Afisa tarafa Nga'pa

d). **Wataalam wasiohudhuria**

Wataalam wote walihudhuria

e).**Waalikwa**

1. Bakari A. Bwatamu - Mwenyekiti CCM (W)
2. Asha Mwendwa - Katibu CCM (W)
3. Shaziry Mohamedi Mosha - Katibu CUF (W)
4. Mohamedi Masoud Katapila - Mwenyekiti CUF (W)
5. Mohamedi Kimwaga - Katibu ACT (W)
6. Said Msusu Amani - M/Kiti ACT (W)
7. Abubakari Hamisi Mkingiye - Afisa Huduma
8. Agnes Akwilini Mnganya - Afisa Huduma
9. Eng. Baraka Mbogora - Mhandisi
10. Mbwana R Kambangwa - Katibu Tawala Wilaya
11. Mosi Ladislaus N - Ag DSO
12. SP Plasius F. Ngaya - OCD
13. INSP Gisela F. Ndunguru - DFO

14. Justine Maingu — DBC
15. SP Alfred P Lemgoha — OI/C Kingurungundwa
16. ASP.Issa Sarota — DIO
17. SP Fadhili J Donile — DPO
18. SSGT Stephen Gasper Kasheta — K/MJAW

**Sekretarieti**

1. Augustino S Augustino Karani wa Vikao.

**HML/BM/MUHT; NA. 13/2022/2023 KUFUNGUA KIKAO**

Kabla ya kufungua Mkutano, Katibu aliwakaribisha wajumbe na waalikwa wote na kuwaeleza kuwa hiki ni kikao cha Pili cha Mkutano wa Pili wa Baraza kwa kipindi cha Robo ya Pili (Oktoba –Disemba),2022/2023.alimkaribisha Mwenyekiti kufungua kikao hicho.Mwenyekiti alikuwashukuru wajumbe wote na waalikwa kwa mahudhurio kisha alifungua kikao hicho mnamo saa 3:32 Asubuhi.

**HML/BM/MUHT; NA. 14/2022/2023 TAARIFA MBALIMBALI TOKA KWA WAGENI WAALIKWA.**

**A.TANESCO**

Ilitolewa taarifa fupi ya utekelezaji wa sghughuli za Tanesco maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ikielezea miradi inayotekelezwa kupitia program za REA. Mtoa mada aliomba wajumbe kutoa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa miradi ya REA kwenye maeneo yao na kuhamasisha wananchi kupisha ujenzi wz miundombinu kwenye maeneo yao bila ya kudai fidia kwani Miradi hiyo haina fidia.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo mwenyekiti alitoa nafasi kwa wajumbe kuuuliza maswali na kutoa maonimbalimbali.**wajumbe walitoa maoni yafuatayo**;

Ilishauriwa kuwa kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi hiyo ni vema viongozi wa maeneo ambayo miradi hiyo inakusudiwa kutekelezwa wapewe taarifa ili kufikisha kwa wananchi mamsuala ya msingi juu ya miradi hiyo.

Aidha ilishauriwa pia wakati wa kuandaa michoro ya maeneo miundombinu itakapokuwa inapita ni vema wakandarasi hao wakazingatia michoro hiyo ili kuepuka uharibifu wa mazao zaidi kunakosababishwa na kukosewa michoro.

**B.TARURA**

Taarifa iliwasiishwa ikieleza miradi inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kwamba utekelezaji wa miradi hiyo imefikia 75%.

Baada ya kuwasilisha taarifa hiyo wajumbe walipata nafasi ya kutoa maoni yao ambapo;

Ilishauriwa na Mhe Mchinjita kuwa wakandarasi wa barabara wahakikishe wakati wa ujenzi wa barabara wanahakikisha wanweka miuondombinu ya kupitika wakati wote na uchafu wote uondolewe mara baada ya mradi kukamilika.

Mhe; Yahya Omari alisisitiza kuwepo kwa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa miradi na ni vema kabla ya wakandarasi hawajaanza miradi kuja kuripoti kwa viongozi wa kata ili viongozi hao waweze kufahamu kinachofanyika na kukisemea kwa wananchi.

Mhe Niger aliomba kujengwa kivuko katika barabara ya Polisi hadi Mdenga ili kurahisisha mawasiliano ya mitaa hiyo.

Mhe Namwete alishauri daraja la kijiji cha Mtumbikile kuzibua matundu ili kurahisisha mawasiliano.

**HML/BM/MUHT; NA. 15/2022/2023 MASWALI YA PAPO KWA PAPO**

Mhe, Meja Kibido Selemani alitaka kujua Lini Halmashauri itatengeneza /kuboresha barabara ya Kilolambwani ilielezwa kuwa Barabara zote zipo chini ya TARURA na Majibu yalikwisha tolewa na Meneja wa TARURA.

Mhe Semeni Juma Ally alishauri kuwa ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa wataala wa ugani ni vema Halmashauri ikatengeneza vipeperushi kwa ajili ya kutoa elimu kwa njia hiyo.ushauri huo ulizingatiwa na menejiment.

Mhe Athumani Mmaije alitaka kujua kama msitu wa makangala amabo ulikuwa na mgogoro na Halmashauri ya Mtama kama umekwisharejeshwa Manispaa ya Lindi .ilielezwa bado suala hilo lipo mamlaka ya Mkoa na linaendelea kufuatiliwa, kwa sasa bado Halmashauri ya Manispaa inatumia rasilimali hizo kupata mapato.

Mhe Asina Kawanga alitaka kujua Mpango wa Halmashauri katika kuhakikisha miundombinu chakavu ya shule inakarabatiwa; alishauri pia ili kukabiliana na uhaba wa madawati ni veam rasilimali Misitu iliyopo Halmashauri ya Manispaa ikatumika kwa kuomba kibali cha kupasua mbao za kutatua tatizo hilo;ilielezwa kuwa kwa sasa Menejiment inachakata Bajeti ya 2023/2024 ni suala la miundombinu chakavu itawekewa katika katika bajeti ili ipate fedha za kukarabati.na kuhusu uhaba wa madawati na samani zingine Halamashauri imepanga kuboresha karakana ili iweze kutumika kutengeneza samani hizo.

Mhe Abed Abed alishauri Fedha za Mfuko wa Elimu ziombewe kibali cha kutoa kiasi cha Fedaha ambazo zitatumika kama dharura kununua mahindi ambayo yatatumika kwenye shule za msingi na sekondari kwa kipindi hiki kigumu ili kuwapatia wazazi nafuu kwa miezi hii ya kilimo.ilielezwa fedha hizo zina maelekezo maalum hivyo wazazi waendelee kuahamasishwa kuchangia chakula kwa watoto wao ili wapate chakula mashuleni.

**HML/BM/MUHT; NA. 16/2022/2023 HOTUBA YA MSTAHIKI MEYA/ MKURUGENZI WA MANISPAA**

Hotuba hiyo ilitolewa ikihimiza ushirikiano baina ya wataalam na wajumbe na wadau wengine ili kuhakikisha ustawi wa jamii ya Halmashuri ya Manispaa inaboreshwa. Kuhakikisha mikopo ya vikundi vya wanawake vijana na walemavu inatolewa kwa mujibu wa miongozo.

**HML/BM/MUHT; NA. 17/2022/2023 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA ROBO YA KWANZA CHA TAREHE 28/10/2022.**

Muhtasari huo uliwasilishwa katika Mkutano huo kwa ajili ya kuthibitishwa, Mwenyekiti aliwapitisha wajumbe ukurasa kwa ukurasa kwa ajili ya masahihisho. Hata hivyo hakukuwa na masahihisho yoyote. Baada ya hapo, Muhtasari huo ulisainiwa na kuwa kumbukumbu halali za Mkutano.

**HML/BM/MUHT; NA. 18/2022/2023 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 28/10/2022.**

Hapakuwa na yatokanayo

**HML/BM/MUHT; NA. 19/2022/2023 KUPOKEA TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA HALMASHAURI/ KUJIBU MASAWALI**

Taarifa kutoka kamati za kudumu za Halmashuri ziliwasilishwa na wenyeviti wa kudumu zikiwa na Agenda zilizojadiliwa kwenye kila kamati husika na maoni yaliyotolewa. Aidha agenda iliyojadiliwa katika kamati ya Ukimwi kwa kipindi hicho ilikuwa ni Utekelezaji wa Shughuli za ukimwi,na kutoa maoni manne. kamati ya Mipamgomiji ilijadili taarifa ya Idara za Mipangomiji,Mazingira na Ujenzi,na kutoa maoni matano,kamati ya Uchumi ilijadili .Utekelezaji Miradi ya Maendeleo na Shughuli za Kawaida na kutoa maoni kumi, Kamati ya Fedha ilijadili Taarifa za Mapato na Matumizi kwa mwezi Juni,Julai na Septemba 2022/2023,Mpango na Bajeti wa 2022/2023,Taarifa ya Mkaguzi wa ndani,Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Shughuli za Kawaida na ilitoa maoni saba.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hizo kwa kila kamati wajumbe walipata nafasi ya kuuliza maswali ambapo Mhe Hussein Kimbyoko alihoji kuhusu fedha za ufuatiliaji wa miradi ngazi za chini kama zinatengwa na nani anawajibu wa kufanya ufuatiliaji ambapo ilijibiwa kuwa ni Idara ya Mipango ndio inayoratibu na kufuatilia.baada ya hapo wajumbe walikubaliana na maoni yaliyotolewa kwa kila kamati na kuzitaka kamati hizo kufuatilia utekelezaji wake.

**HML/BM/MUHT; NA. 12/2022/2023 SALAAM TOKA SERIKALI KUU**

Mkuu wa Wilaya ya Lindi Mhe Shaibu Ndemanga alimshukuru Mwenyekiti kwa mwaliko,alimshukuru pia Rais wa Serikali ya awamu ya sita Dkt Samia Suluhu Hassani kwa kumuamini na kumteua tena kutumikia wananchi kwa nafasi ya Mkuu wa Wilaya, na kumbakisha tena Wilaya ya Lindi,aliomba ushirikiano kwa wadau wote,na kusisitiza yafuatayo; kufuatilia wanafunzi wote wa kidato cha kwanza na darasa la Awali na la kwanza ili waripoti

shule walizopangiwa, kufuatilia na kuhamasisha wananchi kulima mazao yanayostahimili ukame, na mwisho aliwataka wataalam kutekeleza yaliyoshauriwa kwa manufaa ya wananchi.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa aliwajulisha wajumbe juu ya program ya TAKUKURU rafiki na malengo ya uanzishwaji wake na makundi yatakayohusika, aliwataka wajumbe kwenda kuwaandaa wananchi.

Wenyeviti wa vyama Rafiki vya CUF na ACT walipongeza kazi zinazofanywa na Serikali ya awamu ya sita kwa kufungua Demokrasia.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya aliwapongeza vyama rafiki kwa kukubali kazi inayofanywa na Serikalai ya CCM na kuwataka wafanye siasa ya maendeleo,alisistiza wataalam kutekeleza yaliyoagizwa,na alikataa kufanya siasa katika jinai.

**HML/BM/MUHT; NA. 12/2022/2023 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na waalikwa kwa kushiriki kikamilifu siku zote mbili za vikao hivyo, aliwataka wajumbe kujiandaa kwa vikao vya Bajeti Mwisho alifunga Mkutano wa Pili wa Baraza la Madiwani mnamo saa 8:26 Mchana.

**UMETHIBITISHWA NA**

..............................

Juma A. Mnwele
**Katibu**

..............................

Frank Magali
**Mweyekiti**

Tarehe ....20 Mei, 2023....

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

# MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA BARAZA LA MADIWANI KUJADILI MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KILICHOFANYIKA TAREHE 04 FEBRUARI, 2023

## MAHUDHURIO

a) **Wajumbe waliohudhuria**

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mh. Frank Magali | Mstahiki Meya | Mwenyekiti |
| 2. Mh. Salum Bakari Ng`ondo | Naibu Meya | |
| 3. Mh. Nyanga M. Nyanga | Diwani | Tandangongoro |
| 4. Mh. Khalfan M. Mandanje | Diwani | Kata ya Nachingwea |
| 5. Mh. Asina Y. Kawanga | Diwani | Kata ya Msinjahili |
| 6. Mh. Mwanajuma Amiri | Diwani | Viti Maalum |
| 7. Mh. Lunda J. Lunda | Diwani | Kata ya Makonde |
| 8. Mh. Jumu A. Ndondi | Diwani | Viti Maalum |
| 9. Mh .Mwanaidi D. Mbungo | Diwani | Kata ya Ng`apa |
| 10. Mh. Athuman I. Mmaije | Diwani | Kata ya Rutamba |
| 11. Mh. Yahya O.Mohamed | Diwani | Kata ya Mvuleni |
| 12. Mh. Zuhura B. Matindila | Diwani | Kitomanga |
| 13. Mh. Kasim A. Namwete | Diwani | Kata ya Kilangala |
| 14. Mh. Hussein S. Kimbyoko | Diwani | Kata ya Milola |
| 15. Mh. Meja K.Seleman | Diwani | Kata ya Kilolambwani |
| 16. Mh. Abdallah O. Mtambule | Diwani | Kata ya Kiwawa |
| 17. Mh. Asha Y. Mkukulu | Diwani | Viti Maalum |
| 18. Mh. Sharifa S. Kambanga | Diwani | Viti Maalum |
| 19. Mh. Esha S. Mpwaga | Diwani | Viti Maalum |
| 20. Mh. Niger C Mpetula | Diwani | Kata ya Mingoyo |
| 21. Mh. Said M. Mchinjita | Diwani | Kata ya Mnazimmoja |
| 22. Mh. Abeid B. Abeid | Diwani | Kata ya Mtanda |
| 23. Mh. Kitutuma A. Abdurahman | Diwani | Kata ya Rahaleo |
| 24. Mh. Mariam S. Chande | Diwani | Kata ya Wailes |
| 25. Mh. Idd Ngunde | Diwani | Kata ya Matopeni |
| 26. Mh. Paul L. Mapunda | Diwani | Kata ya Mwenge |

| | | |
|---|---|---|
| 27. Mh. Abdallah N. Thabit | Diwani | Kata ya Mbanja |
| 28. Mh. Rashid S.Rashid | Diwani | Kata ya Jamhuri |
| 29. Mh. Seleman T Laus | Diwani | Kata ya Mitandi |
| 30. Mh. Fatuma A. Said | Diwani | Kata ya Chikonji |
| 31. Mh. Abdallah Kikwei | Diwani | Kata ya Rasbura |
| 32. Mh. Juma S. Mpendakulya | Diwani | Kata ya Ndoro |
| 33. Mh. Seif Said Njenga | Diwani | Kata ya Mipingo |
| 34. Mh. Mswalile I. Ally | Diwani | Kata ya Mchinga |
| 35. Mh. Twahil A. Mpuluji | Diwani | Kata ya Matimba |
| 36. Mh. Zainabu Fundi | Diwani | Viti Maalum |
| 37. Mh. Hamida I. Mnunguye | Diwani | Viti Maalum |
| 38. Mh. Fatuma Seleman Ussy | Diwani | Viti Maalum |
| 39. Mh. Ashiza Abdallah | Diwani | Viti Maalum |
| 40. Mh. Zahara Hassan | Diwani | Kata ya Mikumbi |
| 41. Mh. Semeni J. Ally | Diwani | Viti Maalum |

b) **Wajumbe wasiohudhuria**

| | |
|---|---|
| 1. Mhe, Salma Rashid Kikwete | Mbunge Jimbo la Mchinga – kwa taarifa |
| 2. Mhe, Hamida Abdallah | Mbunge Jimbo la Lindi Mjini – Kwa taarifa |

c). **Wataalam waliohudhuria**

| | |
|---|---|
| **1.** Ndg. Juma Mnwele | Mkurugenzi wa Manispaa - Katibu. |
| **2.** Mwandishi L Nchimbi | Mkuu wa Idara ya Mipango,Uratibu na Takwimu. |
| **3.** Dkt Stanford Mwakatage | Mkuu wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Huduma ya Lishe. |
| **4.** Seif A.S | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Taka na Usafi wa Mazingira. |
| **5.** Imani Komba | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. |
| **6.** Rehema Nahale | Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari. |
| **7.** Alex Mkwango | Kaimu Mkuu wa Idara ya Elimu ya Awali na Msingi |
| **8.** Nasri rashidi | Afisa Habari. |
| **9.** Gilya Nyanda | Afisa Mifugo. |
| **10.** Emmanuel Lweyo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Utawala na Usimamizi Rasilimali watu. |
| **11.** Dkt. Idd Ninzar | Kaimu Afisa Mifugo na Uvuvi wa Manispaa |
| **12.** Herry Sanga | Mchumi |
| **13.** Eng. Nestor Chialo | Kaimu Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Miundo Mbinu Vijijini na Mjini |
| **14.** Yusta Msindo | Afisa Mipango |
| **15.** Sharifa Mkwango | Afisa Tarafa Lindi Mjini |
| **16.** Augustino B Chiwinga | Kaimu Afisa Tarafa Milola |
| **17.** Yazidu Mwenda | Kaimu Afisa Tarafa Mipingo |

| | |
|---|---|
| 18. Saidi C Mkingie | Kaimu Afisa Tarafa Nangaru |
| 19. William Mwango'nda | Kaimu Afisa Tarafa Mchinga |
| 20. Christina Chiwanga | Kaimu Afisa Tarafa Mingoyo |
| 21. Justin Sabas | Kaimu Afisa TEHAMA |
| 22. Abdallah Chialo | Afisa Tarafa |
| 23. Florence Kalimwa | Kaimu Mkuu wa Idara ya Usimamizi wa Manunuzi |
| 24. Matilda Luvanda | Afisa Elimu Msingi wa Manispaa |
| 25. Salehe Mohamedi | Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma ya Sheria |
| 26. Ezekiel Sumbuka | Mkuu wa Idara ya Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira. |
| 27. Kyssima D.A | Mratibu wa TASAF |

**c). Wataalam wasiohudhuria**

| | |
|---|---|
| 1. Anandumi Ulomi | Mkuu wa Idara ya Fedha na Uhasibu |
| 2. Faidha Kassimu | Mkuu wa Idara ya UKaguzi wa Ndani |
| 3. Raphael Mauna | Mhasibu Mapato |
| 4. Donald Mwakatundu | Kaimu Mkuu wa Idara ya Biashara,Viwanda na Uwekezaji |

**d). Waalikwa**

| | |
|---|---|
| 1. Bakari Ally Bwatamu | Mwenyekiti CCM (W) |
| 2. Asha Mwenda | Katibu CCM (W) |
| 3. Herieth Raymond Kaluwa | Kaimu Katibu Tawala Wilaya |
| 4. SP Alfred P Lemgoha | Afisa Incharge wa Gereza Kingurungundwa |
| 5. INSP Stella A Meela | Insp |
| 6. SP J A Mbilikira | Kaimu Kamanda wa Polisi Wilaya |
| 7. Mohamed Kimwaga | Katibu ACT Wazalendo |
| 8. Rafiq Mohamedi Ghazal | Katibu TASPA |

**c). Sekretarieti**

Augustino S Augustino

**HML//BMM/BJ.2023/2024/MUHT; NA 01/2022/ 2023 KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alianza kwa kueleza kuwa, kikao hiki ni maalum kwa ajili kujadili Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024. Ilielezwa kuwa Rasimu ya Mpango na Bajeti inayowasilishwa leo imepitia vikao vyote vya kudumu vya Halmashuri na kile cha Baraza la Wafanyakazi na kupata maoni mbalimbali ambayo yamezingatiwa na kuwekwa katika Rasimu inayowasilishwa kulingana na vipaumbele vya Halmashauri kama mtakavyojionea.Baada ya maelezo hayo alimkaribisha Mwenyekiti ili afungue kikao. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe na wataalam kwa mahudhurio mazuri na

kuwataka wawe makini katika kuchangia kila hoja itakayo kuja mbele ya kikao hicho. Baada ya kueleza hayo, alifungua kikao saa 3:45 Asubuhi

**HML//BMM/BJ.2023/2024/MUHT; NA 02/2022/2023 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA AGENDA**

Agenda nne ziliwasilishwa kwa ajili ya kuthibitishwa ambazo ni;

1. Kufungua Kikao.
2. Kupokea na Kuthibitisha Agenda.
3. Kujadili na Kupitisha Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Mwaka 2023/2024.
4. Kufunga Kikao.

Baada ya Kuwasilishwa agenda zote nne zilithibitishwa kwa ajili ya kujadiliwa.

**HML//BMM/BJ.2023/2024/MUHT; NA 03/2022/ 2023 KUJADILI NA KUPITISHA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

Ilielezwa kuwa, Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umeandaliwa kwa kufuata na kuzingatia ukomo wa bajeti wa mwaka 2023/2024 na kwa kuzingatia maelekezo na miongozo mbalimbali ikiwemo;Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya 2020/2025,Hotuba ya Mhe. Rais wakati akizindua Bunge la 13 na maelekezo ya Mhe. Waziri Mkuu,Sheria Na. 9 ya Serikali za Mitaa kifungu cha 13 na marekebisho ya mwaka 2002,Sheria ndogo za Halmashauri, Mpango wa Muda wa Kati yaani MTEF,Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2030,Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA I, mbali na miongozo hiyo ilitajwa miongozo mingineyo iliyotumika kuandaa Mpango na Bajeti hiyo.

**VIPAUMBELE VYA HALMASHAURI KWA MWAKA 2023/2024**

**Kukuza Uchumi wa Wananchi;** Katika eneo hili, maeneo ya kipaumbele yatalenga kutekeleza miradi itakayosaidia kukuza Pato la Wananchi wa Manispaa ya Lindi. Maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2023/2024 ni pamoja na;

i. Kilimo chenye tija kwa mazao ya Korosho, Ufuta na Alizeti.
ii. Kuimarisha mfumo wa minada ya Mifugo na mazao ya Bahari
iii. Kutenga maeneo kwa ajili ya Wajasiliamali wadogo
iv. Kusimamia na kuendeleza Sera ya Mipango Miji na Makazi bora.
v. Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

**MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 – 2025/26**

Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi umeandaliwa kwa kufuata na kuzingatia ukomo wa bajeti wa mwaka 2023/2024 na kwa kuzingatia maelekezo na miongozo mbalimbali kama kama vile;Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya 2020/2025,Hotuba ya Mhe. Rais wakati akizindua Bunge la 13 na maelekezo ya Mhe. Waziri Mkuu,Sheria Na. 9 ya Serikali za Mitaa kifungu cha 13 na marekebisho ya mwaka 2002,

Aidha miongozo mingine iliyotumika ni pamoja na Sheria ndogo za Halmashauri ,Mpango wa Muda wa Kati yaani MTEF,Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2030,Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA I,Mpango Mkakati wa Halmashauri,Mbinu ya upangaji Mipango ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD),Mpango wa Maendeleo wa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi wa miaka mitatu 2023/24 – 2025/26 ,Sera mbalimbali za ki-Sekta,Vipaumbele vya Mkoa na Wilaya,Mwongozo wa Mpango na Bajeti na Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 awamu II kuanzia mwaka 2023/24 – 2027/28,Mpango wa lipa kwa matokeo (EP4R),Mpango wa kuboresha elimu ya sekondari (Secondary Education Quality Improvement Program (SEQUIP)),Takwimu za LGMD na Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi 2022,Sheria ya bajeti No.11 ya mwaka 2015 na kanuni zake.

**Miradi iliyotekelezwa kwa fedha za Mapato ya ndani kwa mwaka 2020/2021**

Kati ya Tshs **2,041,098,450** zilizokusanywa kutoka katika Mapato ya ndani, Tsh **492,698,167** sawa na **40**% zilielekezwa katika miradi kwa sekta za Elimu, Afya, Kilimo, Maendeleo ya Jamii na Utawala.

Kati ya Tshs **2,041,098,450.00** zilizokusanywa ukiondoa vyanzo fungiwa kutoka katika Mapato ya ndani, Tshs **85,149,768.00** sawa na **9.2%** zilitolewa kwa ajili ya ukopeshaji wa vikundi vya wanawake na vijana. Aidha zilitajwa changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya 2020/2021 pamoja na namna zilivyotatutliwa.

**MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2021/2022 KUANZIA MWEZI JULAI 2021 HADI JUNI 2022.**

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Halmashauri ya Manispaa wa Lindi ilikisia Kukusanya na kutumia jumla ya Tsh. **35,094,398,639.62**. Tsh. **592,080,568.40** matumizi ya

kawaida, Tsh.**16,604,209,232** Mishahara, Tsh. **15,047,977,839.62** Miradi ya maendeleo na Tsh. **2,850,122,000**. Kutoka Mapato ya ndani.

**Mapato**

Kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022, jumla ya Tsh **23,153,278,383.42** sawa na **65%** ya Makisio zimekusanywa.

**Matumizi**

Kwa kipindi chote cha kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Juni 2022, jumla ya Tsh **20,100,162,418.64** sawa na **88%** ya Makisio ya makusanyo zimetumika katika utekelezaji wa Shughuli mbalimbali zilizopangwa.

Kati ya Tshs **2,498,481,081.**18 zilizokusanywa kutoka mapato ya ndani Tshs **1,912,611,924.48** kutoka mapato halisi ambapo kati ya fedha hizi **Tsh 600,220,098.38** sawa na asilimia **31%** ya uchangiaji katika miradi ya maendeleo zimeelekezwa katika miradi kwa sekta za Elimu, Afya, Kilimo, Maendeleo ya Jamii na Utawala.

Kati ya Tshs **1,912,611,924.48** zilizokusanywa katika mapato ya ndani Jumla ya Tshs **112,000,000.00** zimewekwa kwenye akaunti ya Mfuko kwa ajili ya vikundi 38 vya vijana, wanawake na wenye ulemavu sawa na asilimia **11%;** ukiondoa mapato lindi wa ( Tshs **242,585,799**).

Aidha yalielezwa mafanikio mbalimbali yaliyopatikana kwa kila idara na kitengo kwa mwaka wa fedha ulioshia Juni 2022.

hata hivyo pamoja na mafanikio hayo zilitajwa pia changamoto za utekelezaji wa bajeti kwa kipindi hicho na njia ambazo zilitumika kutatua changamoto hizo.

**MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2022/2023 KUANZIA MWEZI JULAI 2022 HADI DISEMBA 2022**

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Halmashauri ya Manispaa wa Lindi ilikisia Kukusanya na kutumia jumla ya Tsh. **24,767,395,000.00**. Tsh. **608,701,000.00** matumizi ya kawaida, Tsh.**13,165,578,000** Mishahara, Tsh. **7,858,116,000.00** Miradi ya maendeleo na Tsh. **3,135,000,000.00** Mapato ya ndani.

**Mapato**

Kuanzia mwezi Julai 2022 hadi Disemba 2022, jumla ya Tsh **13,237,905,566.18** sawa na **53%** ya Makisio zimekusanywa.

Kati ya Tshs **1,430,111,077.17** zilizokusanywa kutoka mapato ya ndani Tshs **850,067,436.12** kutoka mapato halisi ambapo kati ya fedha hizi **Tsh.356,580,807.00** sawa na asilimia **42%** ya uchangiaji katika miradi ya maendeleo zimeelekezwa katika miradi kwa sekta za Elimu, Afya, Kilimo, Maendeleo ya Jamii na Utawala. Zilitajwa shughuli hizo zilizotekelezwa.

## UMBILE LA MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24 – 2025/26

Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Halmashauri ya Manispaa wa Lindi inakisia Kukusanya na kutumia jumla ya **Tsh 26,081,127,916.64** kwa mchanganuo ufuatao. **Tsh. 608,701,000.00** Matumizi ya kawaida, **Tsh.13,305,484,079.00** Mishahara, **Tsh.7,858,116,000.00** Miradi ya maendeleo na **Tsh. 3,869,649,525.74** ni mapato ya ndani.

Kutokana na mapato ya ndani ya Tshs **3,869,649,525.74** zitakazokusanywa, Tshs **3,143,899,525.74** Baada ya kuondoa vyanzo fungiwa. (Tshs) **1,257,559,810.30** zimetengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na Tshs **314,389,952.57** sawa na asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani zimepangwa kwa ajili ya mfuko wa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

**Miradi itakayotekelezwa kwa Fedha za Mapato ya Ndani**

Ilitajwa miradi 16 ambayo itatekelezwa kwa kila Idara na vitengo kupitia Bajeti ya mwaka 2023/2024 kwa kuzingatia vipaumbele vya kisekta kupitia Mapato ya ndani.

## MAOMBI MAALUM YA HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI

Ilielezwa kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ni miongoni mwa Halmashauri Kongwe hapa nchini ilibadilishwa kutoka Halmashauri ya Mji wa Lindi kuwa Halmashauri ya Manispaa ya Lindi mnamo tarehe 01,Julai. 2010. Jengo hili la Halmashauri limejengwa mwaka 1955 na lilizinduliwa na Governor wa Mwisho wa Uingereza Sir Edward Twining mwaka 1956 kwa madhumuni ya utoaji huduma kwa wananchi kwa wakati huo wa ukoloni. Pamoja na ukongwe wake bado haina uwezo wa kutosha kuiwezesha kukusanya mapato ya ndani na kuweza kuteleza miradi mikubwa kama jengo la Halmashauri na ununuzi wa gari kwa ajili ya shughuli mbalimbali za Halmashauri.

Kupitia fursa iliyotolewa na Hazina ya kuzisaidia Halmashauri ambazo bado uwezo wake sio Mkubwa katika kukusanya mapato yake ya ndani, Halmashauri ya Manispaa ya Lindi inaomba kupewa fedha. kwa ajili ya Kufanya yafuatayo:-

| NA | MRADI | FEDHA HITAJIKA |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Manispaa ya Lndi | 2,700,000,000.00 |
| 2 | Maombi ya ununuzi wa gari la Mkurugenzi wa Halmashauri | 210,000,000.00 |
| 3 | Ujenzi wa shule ya Sekondari Ngongo | 996,000,000.00 |
| | **JUMLA** | **3,906,000,000.00** |

Baada ya Maelezo na ufafanuzi wa kina Mtoa hoja aliwasilisha Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kwa Mwaka wa fedha 2023/2024 yenye jumla ya Tshs 26,081,127,916.64.

Mwenyekiti alikaribisha maoni juu ya bajeti iliyowasilishwa. Wajumbe walipokea Mpango na Bajeti hiyo na kusisitiza zaidi usimamizi wa makusanyo ili kufikia malengo ya utekelezaji wa Bajeti.Kisha Mwenyekiti aliwahoji wajumbe na kuwataka kusema ndio au Hapana kuhusu Mpango na Bajeti ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ya Mwaka 2023/2024 iliyowailishwa. Wajumbe wote waliitikia ndio kuashiria kuwa Mpango na Bajeti hiyo imeafikiwa na kupitishwa..

**HML//BMM/BJ.2023/2024/MUHT; NA 04/2022/ 2023 KUFUNGA KIKAO.**

Mwenyekiti aliwapongeza timu ya wataalam kwa kuwasilisha Bajeti yenye muelekeo nzuri ya utoaji huduma kwa wananchi,alisistiza kushirikiana katika kusimamia Makusanyo ya Mapato ya ndani,kisha alifunga Mkutano huo maalum Mnamo saa 7:28 Mchana.

**UMETHIBITISHWA NA**

........................................
Juma Mnwele
**KATIBU**

........................................
Frank Magali
**MWENYEKITI**

TAREHE ...20... ~~APRIL~~ MEI, 2023

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Baraza la Madiwani

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya **Kudhibiti Ukimwi** kwa Kipindi cha Robo ya tatu (Januari – Machi) ,2022/2023.

Katika kipindi hicho, Kamati ilifanya kikao kimoja.

Agenda zilizojadiliwa na Maoni ya Kamati yameambatishwa katika Ukurasa wa **16**

**Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.**

*Kamati ya* ***Kudhibiti UKIMWI***

**Agenda zilizojadiliwa.**

1. Taarifa ya Utekelezaji wa Shughuli za UKIMWI kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

**Maoni ya Kamati.**

1. Kamati imeshauri kwa Menejimenti kufufua/kuunda kamati za Kudhibiti UKIMWI, Kamati za Mtakuwa na Kamati za ulinzi wa Mtoto katika ngazi za Vijiji, Mitaa na kata na kuzikumbushia majukumu yao ili ziweze kusaidi kufuatilia na kukabiliana na matendo ya ukatili wa kijinsia, utoaji wa msaada wa wathirika wa ukatili wa kijinsia (social psychological support) na kudhibiti matendo maovu ya ukiukwaji wa maadili.

2. Kamati za Ulinzi Shirikisha jamii ngazi ya kata na vijiji zifuatilie na kubainisha watu wanaojihusisha na madangulo na kushirikiana na jeshi la polisi ili kuchukua hatua kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa maadili.

3. Viongozi wa dini wanashauriwa kutumia makongamano yao na mahubiri yao kukemea maadili potofu na kufundisha watoto maadili wakati wa vipindi vya dini mashuleni.

4. Idara ya maendeleo ya Jamii ihakikishe inafuatilia na kupata majina ya vijana na wasichana wanaojihusisha na maadili potofu ili kuwajengea uwezo wa kifikra na kiuchumi na kuondokana na matendo hayo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Baraza la Madiwani

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya **Mipangomiji, Mazingira, na Ujenzi** kwa Kipindi cha Robo ya tatu (Januari –Machi) ,2022/2023.

Katika kipindi hicho, Kamati ilifanya kikao kimoja.

Agenda zilizojadiliwa na Maoni ya Kamati yameambatishwa katika Ukurasa wa 17

**Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.**

Kamati ya **MIPANGOMIJI, MAZINGIRA NA UJENZI**

**Agenda zilizojadiliwa.**

1. Taarifa mbalimbali za utekelezaji Idara ya Ardhi Mipangomiji na Mazingira kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

2. Taarifa ya Idara ya Maendeleo ya Miundombinu vijijini na Mjini kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi) ,2022/2023.

3. Taarifa ya Kitengo cha Taka na Usafi wa Mazingira kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi) ,2022/2023.

4. Taarifa ya Kitengo cha Maliasili na uhifadhi wa Mazingira Kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi) ,2022/2023.

5. Kujadili na Kupitisha Maombi ya kubadilisha matumizi ya viwanja Nane.

**Maoni ya Kamati**

1. Kamati inashauri Menejimenti kuhakikisha inachagua Mitaa na Barabara kwa ajili ya kupanda Miti ya Vivuli ili kustawisha mji.

2. Menejimenti ihakikishe inafanya mkutano na wamiliki wa maeneo ya gezaulole Kata ya Mchinga ili kutoa ufafanuzi na utaratibu wa kisheria juu ya Eneo hilo ili kupisha Upimaji wa Viwanja.

3. Menejimenti ihakikishe inatoa mafunzo kwa wananchi wanaojihusisha na uvunaji wa Asali katika misitu iliyopo Manispaa ili kuwawezesha kuzalisha asali bora.

4. Menejimenti inashauriwa kuhakikisha usafi wa Mfereji wa Bora uliopo kata ya Ndoro unafanywa mara kwa mara kabla ya msimu wa mvua ili kuwezesha maji kutiririka na kuelekea baharini.

5. Menejimenti inaagizwa kuangalia jengo lililokuwa choo cha zamani Stendi kuu ya Mabasi na kutoa mapendekezo ya matumizi ya jengo hilo na kuhakikisha halisababishi kero kwa wananchi.

6. Menejimenti inashauriwa kufuatilia barabara zote zilizoharibika wakati wa mvua na kuwasiliana na TARURA kuomba matengenezo ya Dharura ili kuwezesha mawasiliano na ufuatiliaji mapato.

7. Kamati imeridhia na kupitisha maombi nane ya kubadilisha matumizi ya viwanja kwa waombaji.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

Mheshimiwa Mwenyekiti

Baraza la Madiwani

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya **Uchumi, Elimu na Afya** kwa Kipindi cha Robo ya tatu (Januari –Machi) ,2022/2023.

Katika kipindi hicho, Kamati ilifanya kikao kimoja.

Agenda zilizojadiliwa na Maoni ya Kamati yameambatishwa katika Ukurasa wa 18 na 19.

**Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.**

Kamati ya UCHUMI, ELIMU NA AFYA

**Agenda Zilizojadiliwa.**

1. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Shughuli za Kawaida kwa Vitengo na Idara za Halmashauri kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

***Maoni ya Kamati***

1. Kamati inashauri kwa Menejimenti kuhakikisha Huduma zote zinazotolewa na Halmashauri ya Mtama kwa wananchi wa Manispaa ambazo zilipaswa kutolewa na Manispaa zinarejeshwa na kutolewa Manispaa ili kuondoa usumbufu na gharama za ufuatiliaji kwa wananchi.

2. Menejimenti imeshauriwa kuwafuatilia wakopeshaji Mikopo kwa wajasiriamali wadogo na kuhakiki uhalali wao, kisha orodha ya wakopeshaji wenye vigezo itolewe kwa Madiwani kwa taarifa na kuhakikisha wale wote wasio na vigezo wanafuata Sheria.
3. Kamati inaipongeza na kuishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuipa Halmashauri Mgao wa Fedha Nyingi za Utekelezaji wa Miradi ya Elimu na Afya na inaendelea kuomba kupatiwa Fedha zaidi za Ujenzi wa Miundombinu mbalimbali katika Halmashauri yetu.

4. Menejimenti ihakikishe ujenzi wa Jengo la Ghorofa Eneo la Radio one linaanza kujengwa na kulikamilisha kwa wakati ili liweze kuongeza mapato ya Halmashauri.

5. Menejimenti inashauri Ushirikishwaji jamii na viongozi wakati wa kuibua na kutekeleza Miradi ya Maendeleo na kuchukua hatua kwa wananchi wanaokataa kushiriki shughuli za Maendeleo ya Umma.

6. Menejimenti inashauriwa kuangalia uwezekano wa ujenzi wa Nyumba ya Mwalimu shule shikizi ya Mtaa wa Mkoimba kata ya Nga'pa ili kuwezesha waalimu kuwa na makazi karibu na shule.

7. Kamati inapongeza Serikali kwa kuanzisha program ya ufundishaji Mahili (competence base) ambayo itawezesha watoto kuelewa zaidi badala ya kukariri.

8. Menejimenti inashauriwa kutumia Rasilimali Misitu na Karakana iliyopo ili kupunguza uhaba wa miundombinu ya madawati na Meza shule za Msingi na Sekondari ili kuwezesha wanafunzi kujifunza vizuri.

9. Menejimenti inashauriwa katika mgao ujao wa waalimu wazingatie kumpeleka mwalimu wa kike shule ya msingi Nanyanje.

10. Menejimenti inashauriwa kuweka mipaka kwenye shule za msingi za pembezoni kwa kupanda miti kuzunguka mipaka hiyo.

11. Menejimenti imeagizwa kuwasilisha majina ya wanafunzi watoro wa shule za Msingi na Sekondari kwa viongozi wa kata vijiji na Mitaa ili waweze kuwatafuta na kuhakikisha wanaendelea na masomo hadi kumaliza. Menejimenti imesisitizwa kuwaelekeza watendaji kata kuchukua Hatua dhidi ya wanaosababisha utoro kwa mujibu wa Sheria ya Elimu ya 1975 na Miongozo yake.

12. Menejimenti inashauriwa kuhakikisha Mafunzo kwa wasajiri wa Bima iliyoboreshwa iCHF inatolewa na kuwapatia vitendea kazi vya kisasa ili kuondokana na changamoto zilizopo.

13. Menejimenti inashauriwa Elimu ya Matumizi ya madini joto inaendelea kutolewa kwa wananchi na kuhamasisha wafanyabiashara kuuza madini joto kwenye maduka yao ili wananchi waweze kununua.

14. Menejimenti inashauriwa Mpango wa Serikali wa Kupeleka mahindi ya bei nafuu kata ya Milola usisitishwe hadi pale Msimu wa chakula kipya utakapokuwa tayari ili kupunguza uhaba wa chakula uliotokana na majanga ya wanyama waharibifu na hali ya hewa.

15. Menejimenti inashauriwa kuendelea kufanya ufuatiliaji na utoaji wa Elimu kuhusu ufugaji katika maeneo ya Mjini ili kuondoa kero.

16. Menejimenti imeshauriwa kufungua mabaraza ya wanawake kwenye kata zilizobakika na kuwajengea uwezo.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

Mheshimiwa Mwenyekiti

Baraza la Madiwani

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

Naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya **Fedha na Uongozi** kwa Kipindi cha Robo ya tatu (Januari –Machi) ,2022/2023.

Katika kipindi hicho, Kamati ilifanya kikao kimoja.

Agenda zilizojadiliwa na Maoni ya Kamati yameambatishwa katika Ukurasa wa 20 na 21.

**Mheshimiwa Mwenyekiti naomba kuwasilisha.**

Kamati ya **FEDHA NA UONGOZI.**

**Agenda zilizojadiliwa.**

1. Kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za *Serikali kwa Mwaka 2017/2018 -2019/2020.*

2. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari – Machi),2022/2023.

3. Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na Shughuli za Vitengo na Idara kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari –Machi), 2022/2023.

4. Taarifa ya Manunuzi kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

5. Taarifa ya Mkaguzi wa Ndani kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

6. Taarifa ya Utawala na Usimamizi Rasilimali watu kwa kipindi cha Robo ya Tatu (Januari-Machi), 2022/2023.

7. Kupitisha Majina ya watumishi wanaopendekezwa kupandishwa Madaraja na Vyeo kwa Mwaka 2022/2023 na Taarifa ya Watumishi Hodari kwa mwaka 2023.

8. Ombi la kubadilisha matumizi ya fedha za ujenzi wa matundu 30 ya vyoo shule ya Msingi Kingurungundwa Tsh 33,000,000.00 kujenga Nyumba ya Mwalimu.

9. Ombi la kuidhinisha matumizi ya Kiasi cha Fedha Tsh 48,300,000.00 kwa Ajili ya Ruzuku kaya Masikini kupitia TASAF.

**Maoni ya Kamati**

1. Menejimenti inashauriwa kuwasiliana na RUWASA ili kuwezesha upatikana wa Maji katika shule ya Msingi Ruchemi.

2. Menejimenti ihakikishe Eneo la Shule ya Msingi Ruchemi inaongezwa na Kupanda miti kuzunguka Mipaka yote ya Shule.

3. Menejiment iwasiliane na TARURA ili kufungua Barabara ya Milola hadi Nangaru ili kurahisisha mawasiliano na ufuatiliaji wa wanyama waharibifu (Tembo).
4. Menejimenti ihakikishe uibuaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo inahusisha wadau wote na kuchukua hatua kwa wananchi wanakataa kushiriki shughuli za maendeleo ya Umma.

5. Menejimenti ihakikishe inafuatilia ukamilishaji wa barabara ya Mtange –kibaoni km 1 ili iweze kukamilika kwa wakati.

6. Menejimenti ihakikishe inawasiliana na RUWASA ili kuhakikisha wanaongeza visima vya maji ili kujitosheleza na mahitaji pindi mradi wa NLG utakapoanza utekelezaji.

7. Kamati imeunga mkono majibu ya Menejimenti juu ya Taarifa CAG na inaagiza kufuatilia wadaiwa waliopelekwa polisi ili kujua mwenendo wa uchunguzi. Kamati imesisitiza kupeleka majibu hayo kwa wakati kwa ajili ya uhakiki kabla ya vikao vya Baraza la Madiwani.

8. Menejimenti ihakikishe wataalam wote wanaoendelea kusababisha hoja wanachukuliwa hatua kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma pale inapoonekana wanarudia rudia makosa hayohayo yanayopelekea hoja.

9. Wawekezaji wote waliopewa mashamba ya uzalishaji zao la korosho ambao muda wa makubaliano ya maendelezo umepita na hawajaendeleza, Menejimenti ihakikishe inawatambua na kurejesha mashamba yote yasiyoendelezwa kwa kupitia vikao vyenye maamuzi.

10. Kamati imepongeza Menejimenti kwa kuwatunuku watumishi utumishi hodari na inashauri kuendelea na mpango huo kila mwaka ili kuleta Ari kwa watumishi.